**Kila mtu ana malaika (08) - Matibabu ya ukimwi na magonjwa ya zinaa**
Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**WAHUSIKA:**

PINTO
ANGELA
JET
MGANGA WA KIENYEJI
ANNIE
NESI

**UTANGULIZI**

Karibu tena kwenye kipindi cha sikiliza ujifunze ambapo utasikia ule mfululizo wa mchezo wa kuigiza
"Malaika wa kila mtu" mchezo ambao unayaangazia kwa undani maisha ya vijana na tabia za kuyahatarisha
maisha yao kwenye majanga ya virusi vya HIV na Ukimwi pamoja na maambukizi ya maradhi mengine ya zinaa.

Katika kisa cha saba ulisikia Angela ambaye ni mja mzito amehamia kwa kijana alomtwika mzigo huo
yaani Pinto lakini Pinto haikubali hali yake ya kiafya ambayo inazorota.Je Angela ataweza kumshawishi
Pinto akapimwe virusi vya HIV na kupewa ushauri nasaha kwa hiari?
Na je Jet atakubali hatimae kuachana na tiba za mitishamba ambazo hadi sasa hazijamfaa katika kutibu
maradhi ya zinaa aliyo nayo?

Tega sikio katika kisa hiki cha Nane cha mchezo "Malaika wa kila mtu"

**SURA YA KWANZA: NDANI ASUBUHI**

| | |
|---|---|
| SFX | PINTO ANAKOHOA BILA YA KUPUMZIKA |
| PINTO | Niko sawa Angela! wacha wasiwasi |
| ANGELA | Lakini Pinto unakohoa namna hiyo wasema uko sawa,unatakiwa kwenda hospitali ukapate matibabu ikiwa kikohozi kinapindukia wiki mbili na zaidi. Na wewe umekuwa ukikohoa kwa zaidi ya wiki mbili Pinto. Shika chai ya vuguvugu hii. (Kimya kidogo) Kesho naenda kiliniki ya mjini, nimetumwa kwenye sehemu ya wazazi. |
| PINTO | Una mimba wewe! sio mimi, nakukumbusha labda ukiwa |

| | |
|---|---|
| | unafikiri nitaandamana na wewe. |
| ANGELA | Pinto, nadhani lazima tuzungumze. Kuna mambo inabidi uyajue. Tena sikiliza kwa makini. Usiku ule tulio lala mara ya kwanza uligundua kama nilikuwa bikra? |
| PINTO | Hapana. Sikumbuki chochote, sikusikia kitu mimi. |
| ANGELA | Basi nilikuwa bikra, ulikuwa mwanamme wa kwanza katika maisha yangu na ndio sababu usiku ule ulikuwa wa kipekee kwangu. Lakini... ah ni vigumu kutamka lakini itanibidi niseme tu. Unajua Pinto mwanamke yoyote mjamzito anayekwenda kliniki anaulizwa ikiwa atakubali kupimwa virusi vya HIV. |
| PINTO | Kwa nini? |
| ANGELA | Kwa sababu ikiwa ana virusi vya HIV, daktari anaweza kumpa ushauri juu ya kuchagua njia salama za kujifungua mtoto. Na mimi nilikubali kupimwa nikajaza fomu, kwenye kliniki ya Matula. |
| PINTO | (akikohoa) Wewe? umepima? halafu? |
| ANGELA | Pinto nimeathirika, nina virusi vya HIV. |
| PINTO | (Kwa kigugumizi) Oh Mungu wangu! Basi umeniambukiza sio? Kwa hiyo kikohozi hiki ndo maana yake nimeambukizwa? |
| ANGELA | Pinto, Pinto kwa nini unajifanya mgumu wa kuelewa namna hiyo? Hebu tafakari bwana, nawezaje kuwa nilikuambukiza wakati nilikuwa bikra? Mtu huambukizwa HIV ikiwa ameongezwa damu iliyokuwa ina virusi hivyo - na mimi sijaongezwa damu, au mtu anaweza kuambukizwa akijidunga sindano ambayo imeshatumika kumdunga mtu mwingine aliyeathirika - na mimi sijawahi kufanya hivyo. Wewe ulikuwa na virusi, na unavyo virusi vya HIV ukaniambukiza, na sijui, labda umeshamuambukiza hata mtoto. |
| PINTO | (Na kigugumizi) Unataka kunilaumu tu. Hutaki kukubali kwamba ulilala na mwanamme mwingine, kwa hivyo unanibandikizia mimi. |
| ANGELA | Si kweli hayo unayosema Pinto, wewe ndo ulokuwa wa kwanza kulala na mimi katika maisha yangu na sijawahi kufanya mapenzi na mtu mwingine yoyote, na mimi ninakueleza tu wala sikulaumu. Mtu anayehusika kutoa ushauri na maelezo kuhusu Ukimwi kupitia njia ya simu alinambia.... |

| | |
|---|---|
| PINTO | (Anakatiza) Maelezo kuhusu ukimwi kwa njia ya simu? Mungu wangu. Enhe umezungumza na nani mwingine juu ya haya? |
| ANGELA | Nilitaka kujua Pinto, niamini nimeweka siri habari hizi. hakuna anayejua kama nina virusi, sio mama wala mjomba Billy. Hakuna kati yao anayejua, isipokuwa marafiki zangu wa karibu, lakini hawakuweza kunambia virusi hivi vitakuwa na madhara gani kwangu. Kwa hiyo mshauri kwa njia ya simu akanieleza yote na pia akanikanya nisianze kucheza mchezo wa kulaumiana. Maana itakuwa ni kupoteza muda na nguvu tu, kwa sababu kama ni kuambukizwa nshaambukizwa, nikikulaumu, halafu na wewe ukamlaumu alokuambukiza, itakuwa ni sawa na kuuliza kati ya kuku na yai nani alokuja kwanza? Hakuna kati yetu alotumia kinga ya Condom. Huo ndio ukweli. |
| PINTO | (asita sita) oooh no, sasa tutafanya nini Angela? nifanye nini? |
| ANGELA | Pinto, lazima ujue hali yako juu ya HIV. Unaweza kwenda kupima na kupewa ushauri kwa hiari yaani VCT. Inabidi ujue kuhusu kinga yako ya mwili, inafahamika kama CD4 count au T cell Count. |
| PINTO | (wasi wasi) Sasa ni nini hiyo tena? |
| SFX | SAUTI YA MAKARATASI |
| ANGELA | Angalia, yote hayo yameelezwa hapa kwenye kijitabu hiki. (anasoma) Hiyo inayoitwa T cell count au CD4 count inaonyesha idadi ya chechembe za celli zinazopambana na maradhi ndani ya mwili wako. T celli ni celli ya kipekee ya kupambana na maradhi na unapokuwa nazo nyingi mwilini ndivyo mwili unavyokuwa na nguvu zaidi za kukabiliana na ugonjwa. (anamaliza kusoma) |
| ANGELA | Sasa umeona,watakupima damu kuangalia una kiasi gani cha celli za kinga mwilini, halafu watakupima tena kuhakikisha. Halafu watajua ikiwa wakuanzishie dosi ya dawa za kuongeza nguvu au la. Ndo sababu Pinto ni muhimu kwenda kupima. |
| PINTO | Lakini umeshanambia kila kitu, sasa najua nina virusi vya HIV na maanake ni kwamba nitakufa tu, kwa hivyo sina haja ya kwenda kwenye vipimo vya kipuuzi ambapo ntaambiwa yale yale ambayo nimeshayasikia. |
| SFX | KIKOHOZI KINAFUNGA SURA HII |

## SURA YA PILI: KWA MGANGA

| | |
|---|---|
| SFX | MUZIKI WA KIASILI UKIWA CHINI KWA CHINI |
| JET | Ubaba muwasho umechacha na bado nachomeka tu. Dawa ulonipa imenisafisha vya kutosha,nimeharisha wiki nzima na sasa siwezi tena kuvumilia,nimechoka.. sina hata nguvu |
| MGANGA | Mizimu ya babu zako imekukusirikia wewe,Jet lazima uombe msamaha kweli kweli na tumia dawa hii kujipaka kwenye upele huo umesikia. |
| JET | Nitawaomba mizimu msamaha lakini siitaki tena hiyo dawa Ubaba inachomaa lo,siwezi hata kwenda kazini kwa sababu saa zote nasikia muharoo. |
| MGANGA | Sasa basi kuna kitu kimoja tu ambacho kitakusaidia kukuandikia barua ya kukutuma uende ukatibiwe Matula Kliniki. |
| JET | Lo hapana Ubaba siwezi kwenda kliniki ya Matula afadhali uniandikie nende kliniki ya mjini Ubaba.. |
| MGANGA ; | (Amkatiza) Kwa vile iko mbali, na hutaki watu wakuone, hilo nalijua, nimeshayasikia hayo zamaniii. sawa, barua hii inagharimu shillingi mia 500 keshi. unaweza kulipa? |
| JET | Ndio ninazo, kwanza ndo nilobakia nazo katika mshahara wangu wa mwezi ulopita. |
| SFX | SAUTI YA KARATASI IKIANDIKWA |
| MGANGA | Idara ya afya imekuwa ikijaribu kwa miezi sasa kutafuta ushirikiano na sisi waganga.ili tuwatume wagonjwa wanaokohoa na kuwa na muwasho na dalili kama hizi zako katika kliniki za kiserikali na kwa njia hii tunafurahi sana. |
| SFX | PESA ZIKIHESABIWA, SHILLINGI<br>MUZIKI WA KUFUNGA SURA |

## SURA YA TATU: KLINIKI

| | |
|---|---|
| ANNIE | (Kwenye simu) Angela? niko kwenye foleni ya kuchukua dawa,vipi uko wapi wewe? |
| ANGELA | Nakarbia kuitwa,nitakuja nje sasa hivi kama dakika kumi hivi nipe. |
| ANNIE | Ok basi nitakufuata huko nikimaliza,hebu subiri kidogo namuona Jet anakuja. |

| | |
|---|---|
| ANGELA | Jet? |
| ANNIE | Ndio Jet sikiliya Angela tutaonana nipe dakika moja tu sawa,bye. |
| NESI | Angela Selebi? njoo upande huu tafadhali. |
| SFX | PITA PITA KWENYE UKUMBI, MILANGO YAFUNGULIWA NA KUFUNGWA SAUTI ZA OFISINI, SIMU ZINALIA N. K. |
| SFX | Muziki wa kuunganisha |
| NESI | Kwa hiyo Angela ni muhimu uelewe ni maamuzi gani uliyo nayo kuna sheria mpya sasa hivi katika idara ya afya inayotoa uwezo kwa kliniki hii kuwapa kina mama wenye virusi vya HIV dawa za AZT.Usijali kuhusu jina hilo hii ni dawa ambayo inafanya kazi vizuri katika kipindi cha wiki kadhaa hadi kufikia siku ya kujifungua mtoto, kwa hali kama yako Angela ni muda wa kama wiki kumi kwa hivyo tunaweza kuanza sasa. |
| ANGELA | Sister nataka kujua,je itanibidi kulipia matibabu haya? |
| NESI | Hapana hulipi kitu.hii ni kiliniki ya serikali na kampeini ya kupigia debe kuanzishwa kwa huduma ya dawa za kupunguza makali ya virusi vya HIV inamaanisha dawa hizo zitolewe bure. Una bahati sana Angela kwa kuwa unaishi hapa karibu.wajua wanawake wengi wa vijijini hawapati huduma hii na wala hawajapata kuisikia. |
| ANGELA | Niliona jinsi watu walivyokuwa wapiga foleni katika kliniki ya Matula.wanasubiri kwa siku nzima na wala hawapati huduma zenyewe wanaambulia patupu. |
| NESI | Nimegundua kwamba matibabu hayalingani lakini unaweza kukutibu mradi tu uelewe Angela kwamba hatuwezi kukuponya.matibabu haya ni ya kukusaidia tu kukuongezea chembechembe za celli mwilini za kupambana na maradhi yaani CD4. lakini pia chembechembe hizo bado zinaweza kupungua ikiwa utapata maambukizi mengine. Tunachoweza kukifanya ni kupunguza kabisa uwezekano wa kumuambukiza mtoto wako virusi vya HIV kwa kuwapa nyote wawili hii dawa inayopambana na virusi hivyo. |
| ANGELA | Utafanya vipi? |
| NESI | Wakati wa kujifungua utapewa kidonge kimoja cha dawa ya Nevirapine na mtoto pia atapewa kimoja mara tu atakapozaliwa.halafu nyote wawili mtakuwa mkiendelea |

kutumia dawa nyingine za kupunguza makali ya virusi za AZT, kwa muda wa siku saba baada ya kujifungua. Mwanao atapimwa virusi katika wiki sita na wakati atakapokuwa na miezi 18.

ANGELA Na je inawezekana akazaliwa bila virusi wakati sisi tumeathirika?

NESI Ndio inawezekana.tunajaribu kupunguza kiwango cha maambukizi ya HIV kutoka kwa mama hadi kwa mtoto kufikia chini ya asilimia 5

ANGELA Na ikiwa nataka kumnyonyesha mwanangu?

NESI Hapo inabidi uwe mwangalifu na umnyonyeshe matiti tu kwa miezi sita na usichanganye chakula kingine,maziwa ya mkebe au hata maji kwa mtoto kwa sababu ukifanya hivyo unaweza kusababisha mikwaruzo katika tumbo la mtoto ambalo bado ni laini halafu virusi vinaweza kupenya kutoka kwenye maziwa yako ya matiti hadi kwenye damu ya mtoto. Kwa maana hiyo chagua aidha kumnyonyesha matiti tu au kumpa maziwa ya dukani tu kwa muda wa miezi sita.

ANGELA Bora nimnyonyeshe matiti Sister.

NESI Sawa, na umeshaamua kuhusu njia ya kujifungua mwanao, utapendelea kujifungua kwa njia ya kawaida au upasuaji?

ANGELA Kwanini,kwani njia ya kupasuliwa ndo ina punguza hatari ya maambukizi kwa mtoto?

NESI Unajua Angela, ukipasuliwa inamaanisha mtoto atatolewa bila ya wewe kusukuma ambapo pengine uvuje damu nyingi ndani kwa ndani na umkwaruze mtoto wakati ukisukuma.Virusi vinaweza kupenya na kuingia kwa mtoto kupitia damu ikiwa utajifungua kwa njia ya kawaida, tumeleewana?

ANGELA Unaeleza vizuri kweli, Sister nimeelewa sana!

NESI Vizuri! Sasa suali jingine, je mnaonana kimapenzi na mwanamme wako? nauliza kwa sababu ulinambia lazima atakuwa ana virusi vya HIV. Kwa maana hiyo Angela, inabidi usisitize matumizi ya Condom au muache kabisa kuonana kimwili. Na uje hapa kliniki baada ya kila miezi sita kwa ajili ya kupima.

ANGELA Lakini Pinto hataki kabisa kuja kupima,anaogopa atakufa, sasa ntamwambia nini Sister?

NESI Mwambie anaweza kuishi na virusi lakini woga ndio unaoua.

## Hitimisho

"Malaika wa kila mtu" ni mchezo wa kuigiza uliotungwa na Romie Singh na kuhaririwa na Saumu Mwasimba. Na hadi hapo ndio tunakamilisha kipindi cha sikiliza ujifunze kwa leo.

Annie amemuona Jet katika kliniki, je atafanya vipi ili akutane nae?
Na Djamila anakabiliana na mjomba wake anayemtongoza! Kwa mengi juu ya mchezo huo, jiunge nasi katika sehemu ya tisa.

Kumbuka ukiwa unataka kusikiliza tena kisa hiki au unataka kuwaambia marafiki wasikilize unaweza kutembelea tovuti yetu kupitia anuani ya www.dw.de/lbe Kwa heri!